CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA VIWANDA, BIASHARA, TAASISI ZA FEDHA, HUDUMA NA USHAURI (TUICO)

CHOMBO HURU CHA WAFANYAKAZI

J I U N G E L E O

T U J I U N G E W O T E

KWA MAISHA YETU BORA

IMETAYARISHWA NA:

OFISI YA KATIBU MKUU,
TUICO MAKAO MAKUU
S.L.P. 5680,
TEL: 255 22 2866910/60
FAX 255 22 2866911
EMAIL: tuico2004@yahoo.com

1.0. MFANYAKAZI NI NANI

Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini na. 6 ya mwaka 2004 na Sheria ya Taasisiz a kazi Na. 7 ya mwaka 2007 zinamtafsiri mfanyakazi kuwa ni mtu yeyote aliyeingia katika mkataba wa ajira wa aina yoyote kumfanyia kazi mtu mwingine kwa ujira. Mtu huyo atakayefanyiwa kazi asiwe mteja wa taaluma yoyote, biashara au kazi inayofanywa na mtu huyo.

- Mfanyakazi pia ni mtu yeoyte aliyetajwa kuwa mfanyakazi na Waziri chini ya kifungu 98 (3) cha Sheria tajwa.

- Sheria zinamfafanua zaidi mfanyakazi kuwa ni mtu anayefanya kazi au anatoa huduma kwa mtu mwingine bila kuangalia aina ya Mkataba iwapo vigezo vifuatavyo vitakuwepo:-

    1. Mfanyakazi anakuwa chini ya uangalizi wa mtu mwingine
    2. Muda wake unaangaliwa na mtu mwingine
    3. Mtu husika ni sehemu ya Shirika/Taasisi
    4. Kufanyakazi kwa uwiano wa masaa 45 kwa mwezi kwa muda wa miezi mitatu
    5. Mtu husika anamtegemea kiuchumi anayemfanyia kazi
    6. Mtu huyo anafanya kazi au kutoa huduma kwa mtu mmoja tu
    7. Mtu husika amepewa vifaa vya kazi na mtu anayemfanyia kazi.

- Ni wajibu wa Mwajiri kisheria kumpatia mfanyakazi taaarifa ya Ajira yake kinyume chake mwajiri anakuwa na wajibu wa kuthibitisha ajira ya mfanyakazi utokeapo mgogoro.

- Katiba ya TUICO inamtafsiri mfanyakazi kuwa ni mtu yeyote aliyeingia mkataba wa kuajiriwa kwa ujira wa wiki au mwezi vile vile mfanyakazi ni mtu yeyote aliyejiari.

2.0. MWAJIRI NI NANI

Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini na. 6 ya mwaka 2004 imemtaja mwajiri kuwa ni mtu yeyote pamoja na Serikali na wakala wa Serikali anayemwajiri mfanyakazi.

Katiba ya Chama ya TUICO imemtaja mwajiri kuwa ni mtu, chombo au mamlaka ambayo imamiliki mali au mtaji katika kampuni, taasisi, Shirika au kiwanda na ameajiri watu kwa madhumuni ya kumfanyia kazi na kuwalipa ujira au malipo.

3.0. CHIMBUKO LA CHAMA CHA WAFANYAKAZI

Tafsiri ya Mfanyakazi na Mwajiri inaonyesha ushirika wa wazi kati ya pande hizi mbili ambao unazaa mahusiano kati yao. Mahusinao kati ya Mfanyakazi na Mwajiri ni ya vuta nikuvute. Wakati mwajiri nataka kupata faida kwa kumtumia mfanyakazi kwa kumfanyisha kazi zaidi kwa maslahi kidogo; mfanyakazi anataka kufanyakazi yenye staha yaani inayojali mazingira na yenye kukidhi maslahi

Mvutano huo katika mahusiano umelazimu Wafanyakazi kujiunga na kuunda Chama cha kusimamia mahusiano na Mwajiri ili kuhakikisha mfanyakazi anafanyakazi yenye staha.

4.0. CHAMA CHA WAFANYAKAZI NI NINI?

Chama cha Wafanyakazi ni chombo huru kinachoundwa na kusimamiwa na Wafanyakazi wenyewe kwa ajili ya Wafanyakazi wenyewe.

5.0. HAKI ZA KIOGANAIZESHENI

Ili Chama cha Wafanyakazi kiweze kuwepo na kutekeleza majukumu yake Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya 2004, Sheria ya Taasisi za Kazi Na. 7 ya 2004 na Kanuni zake zimeainisha haki za kioganaizesheni za Chama cha Wafanyakazi kilichosajiliwa kama zifuatavyo:-

(i) Kuingia eneo la mwajiri kwa ajili ya:-

- (a) Kuingiza Wanachama
- (b) Kuwasiliana na Wanachama
- (c) Kukutana na Wanachama wanapokuwa na masuala yoyote na mwajiri wao
- (d) Kuitisha mikutano na wafanyakazi
- (e) Kusimamia upigaji wa kura kwa mujibu wa Sheria na Katiba ya Chama

(ii) Kuanzisha Tawi sehemu ya kazi ambapo Chama kila wanachama wake kumi au zaidi kati ya waajiriwa.

(iii) Kutambuliwa na Mwajiri kama wakala pekee wa Wafanyakazi katika Majadiliano ya pamoja ikiwa Chama kina wanachama zaidi ya nusu ya wafanyakazi.

(iv) Kupatiwa vitendea kazi muhimu kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za Chama sehemu ya kazi.

(v) Kupatiwa taarifa muhimu ili kuwezesha Majadiliano ya pamoja.

6.0. TUICO NI NINI?

TUICO ni Chama cha Wafanyakazi wa Sekta za Viwanda, Biashara, Taasisi za Fedha, Huduma na Ushauri. Chama kinaongozwa na Katiba na Kanuni ambazo zilipitishwa na Mkutano Mkuu wa Taifa wa TUICO. Chama kilisajiliwa kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Wafanyakazi na kuanza shughuli zake tarehe 1 Januari, 1996 na kusajiriwa tena kwa mujibu wa Sheria ya Ajira na Mahusiano Kazini Na. 6 ya 2004 na kupata Namba ya usajili Na.01. TUICO ni Chama shiriki cha TUCTA na kimejishirikisha na Mashirikisho ya Vyama vya Wafanyakazi Duniani, Afrika na Afrika Mashariki.

7.0. MWANACHAMA NI NANI NA NAMNA YA KUJIUNGA

7.1. MWANACHAMA NI NANI

Katiba ya Chama inatafsiri mwanachama kuwa ni Mfanyakazi aliyejiunga na Chama kwa kulipa kiingilio na kupewa kadi na kukubali masharti ya Chama ikiwa ni pamoja na kulipa michango ya kila mwezi.

7.2. HAKI NA NAMNA YA KUJIUNGA

- Kwa mujibu wa Kifungu cha 9 cha Sheria ya Ajira na Uhusiano Kazini Na. 6 ya mwaka 2004 Mfanyakazi yeyote ana haki ya kuunda na kujiunga na Chama cha Wafanyakazi kwa kujaza Fomu maalum Na. 6.

- Mwanachama wa Chama cha Wafanyakazi ana haki zilizoanishwa katika Katiba, Kanuni na Sheria ikiwa ni pamoja na kushiriki kikamilifu katika shughuli za Chama.

- Uanachama na haki zinawahusu pia wale wanoomba ajira.

- Mtu/Taasisi hairuhusiwi kumbagua/kumnyanyasa mfanyakazi kwa sababu:-

    - Anajihusisha/amejihusisha na haki zake zilizoainishwa na Katiba na Sheria.
    - Ni mwanachama au anakuwa mwachama wa Chama cha Wafanyakazi
    - Anashiriki/ameshiriki katika shughuli za Chama.

- Mfanyakazi kiongozi mwandamizi, ambaye anatafsiriwa na Sheria kuwa mwenye nafasi ya ajira ya kutengeneza sera kwa niaba ya mwajiri, ana mamlaka ya kufanya mikataba ya pamoja kwa niaba ya mwajiri, anaruhusiwa kuwa mwanachama wa Chama cha Wafanyakazi.

8.0. MISINGI NA MADHUMUNI YA CHAMA

8.1. MISINGI YA CHAMA

Chama kinajengwa na hivyo kuonekana kama chombo cha Wafanyakazi kwa misingi ifuatayo:-

- Uhuru
- Umoja na mshikamano
- Demokrasia na Nidhamu
- Uongozi na uwajibikaji
- Mapato ya Chama
- Uwazi na ukweli
- Utawala wa Sheria
- Haki na Wajibu
- Usawa na Heshima

8.2. MADHUMUNI YA TUICO

TUICO dhamira yake ni kujenga Chama imara ili kiweze kutekeleza madhumuni ya uwepo wake kwa Wanachama ambayo ni pamoja na:-

- Kumuelimisha mwanachama kuhusu Sheria za ajira na Katiba ya Chama
- Kumtetea mwanachama dhidi ya dhuluma, uonevu, ubaguzi na migogoro mbalimbali baina ya mfanyakazi na waajiri
- Kufunga mikataba ya hali bora sehemu za kazi kwa lengo la kuboresha maisha ya wafanyakazi
- Kudumisha mahusiano mema baina ya Wafanyakazi, Mwajiri, Chama na Serikali na hivyo kuongeza ufanisi kwa faida ya wahusika wote.
- Kushirikiana na Mwajiri katika kuhakiksha kuwa Wafanyakazi wanafanya kazi katika mazingira safi kiafya na salama
- Kushirikiana na Mwajiri kuhakikisha kuwa makundi maalumu ya wafanyakazi yanapata haki sawa na wanafanya kazi katika mazingira salama

9.0. MANUFAA YA KUJIUNGA NA TUICO

Kwa kuzingatia misingi na madhumuni ya TUICO, manufaa ya kujiunga na TUICO ni pamoja na:-

- Mwanachama kustawi kiuchumi (prosperity)

- Mwanachama kuwa na usalama wa ajira na afya yake pamoja na familia yake (Security)
- Mwanachama kuwa sawa na wengine bila kujali tofauti za elimu na maumbile, kabila, dini n.k. (Equality)
- Mwanachama kuwa na uwezo kukabiliana na maisha hata wakati wa mabadiliko ya kiuchumi na kiteknolojia (Sustainability)
- Mwanachama kuendesha Chama katika misingi ya kidemokrasia na uwajibikaji (Democracy and Accountability)
- Mwanachama kuwa mbunifu katika kazi yake ili kukabili mabadiliko ya kiteknolojia (Innovative)
- Mwanachama kuwa na uwezo wa kuchagua fursa za kimaendeleo zinazojili katika soko la ajira (Choice).
- Kumtetea mwanachama katika migogoro ya kikazi

MSHIKAMANO DAIMA!